AJIRA, USTAWI NA
UJASIRIAMALI

# KUANDAA KIPINDI

# AJIRA, USTAWI NA UJASIRIAMALI
KUANDAA KIPINDI

**MAANDALIZI YA KIPINDI**

## NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZIA AJIRA, USTAWI NA UJASIRIAMALI KATIKA JAMII YAKO

- Ujuzi na mikakati ya kufanikiwa katika njia ya kuchaganya mbinu za ustawi
- Fursa za biashara katika mnyororo wa thamani wa kilimo katika jumuiya yako
- Mtazamo wa kijinsia kuhusu upatikanaji na fursa za ustawi
- Mfumo wa Ustawi Endelevu unajionyeshaje katika jumuiya yako?

**CHAGUA MADA MAHUSUSI**

Fursa za biashara katika mnyororo wa thamani wa kilimo katika jamii yako

## KUKUSANYA UJUZI WA MNYORORO WA THAMANI WA KILIMO KATIKA JUMUIYA YAKO: MASWALI YA KUZINGATIA

- Mnyororo wa kilimo-chakula uko vipi katika jumuiya yako, na unauhusiano gani na fursa za kazi/ajira?
- Ni changamoto gani zinazowakumba vijana zinazohusiana na kutopatikana kwa ardhi, tofauti ya jinsia na mienendo ya vizazi?
- Hali ya kilimo katika jumuiya yako iko vipi? Je, ujuzi wako unaku-unganishaje na fursa zilizopo kwenye mnyororo wa thamani?
- Vijana wanaweza kushiriki vipi katika kila hatua kwenye mnyororo wa thamani?
- Ni vikwazo gani vijana hukumbana navyo katika shughuli za mnyroro wa thamani?
- Kuna fursa mpya zinazojitokeza, mfano kwa upatikanaji na ma-tumizi zaidi ya huduma za pesa kupitia simu?

## MUUNDO WA KIPINDI CHA REDIO

### SAUTI YA UMMA

**Lengo la sauti ya umma**
Kupata maoni mengi juu ya mada moja.

**Ni na nani unayezungumza naye**
Mtu yeyote kutoka kwa jamii

**Swali**
- Unaona fursa zipi katika mnyororo wa thamani wa kilimo katika jumuiya hii?

### MAONI YA SAUTI

**Nia ya ufafanuzi wa maoni ya sauti**
Kupata maoni ya watu juu ya mada am-bayo wanayoijali sana.

**Utazungumza na nani**
Mhadhiri au mkufunzi ambaye anaweza kuelezea mnyororo wa thamani na kutoa taarifa kuhusu baadhi ya fursa zilizopo na jinsi ya kuzipata.

## MUUNDO WA KIPINDI CHA REDIO

### WASIFU WA SAUTI

**Lengo la wasifu wa sauti**
Kupata masimulizi ya mtu aliye na uzoefu au shauku katika jambo fulani. Mara nyingi muundo wa wasifu wa sauti unatumika kwa kuhamasisha wengine.

**Utauliza nani**
Mjasiriamali wa kilimo ambaye anafanya biashara katika mnyororo wa thamani wa ndani, aliyeachana na mifumo ya ukulima wa kujikimu tu, na kuanza kukuza biashara ya kilimo ya kufana. Waulize wazungumzie changamoto na vizuizi walivyopata, na jinsi walivyopambana na kuzitatua; ni nini kinachofanya biashara yao kufana, na wana malengo gani ya kukuza biashara yao.

**Maswali ya kuuliza kabla ya kuanza kurekodi ili kumsaidia mhusika kufikiria wasifu au simulizi yake:**

- Ni nini kilicho fanya utake kuwa 'mjasiriamali' wa kilimo?
- Unasemaje kwa watu wanaofikiri kwamba kilimo sio biashara endelevu?
- Ni aina gani ya changamoto za kifedha au rasilimali ambazo ulikabiliana nazo ukianza?
- Unafikiri ni ujuzi, uelewa, rasilimali na mahusiano gani ya muhimu zaidi kuwa nayo katika biashara yako?
- Je, ni udhaifu upi wa  biashara yako, na unalindaje ustawi wako?
- Ni biashara gani zingine unazofanya katika mnyororo wa thamani, na vipi shughuli zako zinavyosaidia au kujumuisha hizo biashara zengine?
- Washindani wako ni nani na unakabiliana na hali ya ushindani kivipi?
- Je, kuna fursa zipi za biashara za vijana kushiriki katika mnyororo wa thamani?
- Je, maendeleo mapya kama huduma za pesa kwa njia ya simu zinabadilisha mazingira ya kufanyia biashara kivipi??
- Ni ushauri gani unaoweza kumpa kijana anayeanza?
- Je, mawazo yako mwenyewe yamebadilika kuhusu maana ya kushiriki katika kilimo?
- Ni changamoto na fursa zipi mpya ambazo unaona zilijitokeza katika mnyororo wa thamani?

**Tafadhali angalia maswali ya mahojiano katika "Jinsi ya kuandaa kipindi".**

---

### TANGAZO LA UMMA

**Lengo la Tangazo la Umma**
Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

**Unda Tangazo la Umma linalowahimiza watu kuendeleza ujuzi wa ustawi na mikakati inayochangia ustawi wa kaya zao AU unaoboresha uelewa wa hatua tofauti-tofauti zilizopo katika mlolongo wa thamani, na fursa za kujenga ustawi ndani ya mlolongo wa thamani wa kilimo.**

## JINSI YA KUENDESHA KIPINDI

**Tumia vipengele, utafiti wako, muongozo uliyopendekezwa na maswali kuandika muongozo wako mwenyewe sasa.**

[KUFUNGUA KIPINDI:]
**Mtangazaji 1:** Imetimia saa [MUDA] na ni wakati wa [JINA LA KIPINDI] kwenye [JINA LA REDIO]. Jina langu ni [JINA].

**Mtangazaji 2:** Na jina langu ni [JINA], na kipindi cha leo ni juu ya kuelewa nafasi za biashara kwa vijana katika sekta ya kilimo katika jumuiya yetu. Hiyo ni kweli, tutazungumzia mnyororo wa thamani, jinsi unavyofanya kazi na jinsi ya kujihusisha nao kama 'mjasiriamali wa kilimo' .

**Mtangazaji 1:** Hiyo ni kweli, tutazungumzia jinsi ambavyo kilimo kimekuwa fursa kubwa ya biashara. Inahusu zaidi ya kilimo cha chakula cha kujikimu tu. Miji inazidi kukua, na mahitaji ya chakula bora yanazidi kuongezeka. Teknolojia kama huduma za pesa kwa njia ya simu pia zinabadilisha jinsi biashara inavyofanywa, na kufungua fursa mpya kwa vijana. Ukiwa na uelewa kiasi wa biashara, njia ni nyingi za kukuza biashara ya kufana ndani ya mnyonyoro wa thamani.

**Mtangazaji 2:** Leo tutazingatia jinsi vijana wanaweza kujiingiza kwenye mnyororo wa thamani ya kilimo, na kuelewa aina ya ujuzi na rasilimali ambazo zinahitajika ili kuweza kufana, pamoja na hatari za kuanzisha biashara yako mwenyewe. Tunakuletea taarifa muhimu zinazohitajika ili kuanza mazungumzo ya kuwa mjasiriamali wa kilimo aliyefana.

**Mtangazaji 1:** Hebu tusikie zaidi kuhusu kile ambacho watu wanafikiria kuhusu fursa za biashara zilizopo katika mnyororo ya thamani wa kilimo.

[TAMBULISHA MGENI ANAYEHOJIWA]
[CHEZA MAHOJIANO]

[FUNGA KIPENGELE]
**Mtangazaji 1:** Leo tumejifunza juu ya mnyororo wa thamani na jinsi inavyowezekana kuunda biashara ya kufana katika kilimo.

**Mtangazaji 2:** Ndiyo, hiyo lilikuwa ya kuhamasisha. Sekta ya kilimo inabadilika kwa njia nyingi, na ni vizuri tumeweza kusikia kuhusu jinsi vijana ambao ni wajasiriamali wa kilimo wanaweza kuchangia kutoa chakula cha afya na cha bei nafuu kwa idadi ya watu inayozidi kuongezeka, na kupata pesa kutokana na huu ujasiriamali!

**Mtangazaji 1:** Hadi wiki ijayo, siku ya [TAJA SIKU] saa [MUDA]. Tutazungumza kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri kutoka kwetu!

## MUUNDO WA KIPINDI




### MAADILI NA IDHINI/ RIDHAA

Hakikisha umewafahamisha wasikilizaji kuwaheshimu wale wanaotoa hadithi zao za kibinafsi.

### MPANGILIO WA SHUGHULI ZA KUFIKIA JAMII

Unapopanga shughuli yako ya kufikia jamii, tahadhari nishati ambayo shughuli
fulani huzalisha ili uepuke kuanza kwa kishindo na kisha kumalizia kwa wepesi.